WADAU NA SERIKALI WAMECHUKUA HATUA GANI KUKOMESHA AJIRA ZA WATOTO MIGODINI

Kutoka kwenye sera ya Taifa ya watoto ya mwaka 1996 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2008 imeweka bayana muundo unaolenga kumpa kinga na viwango ili kutoa haki kwa watoto, kanuni za kuthibiti ajira kwa watoto pia zimepewa nguvu zaidi katika sheria hii.

Vitendo vya utumikishaji wa watoto vinapingana na sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo si tu kwamba imefafanua haki za watoto katika mazingira mbalimbali, bali imeweka vifungu vinavyoainisha wajibu wa watendaji, wakiwemo wazazi katika kuwalinda na kuwajali watoto.

Kifungu cha 9 cha sheria hiyo kinaainisha wajibu wa wazazi kwa watoto wao ingawa vipo vifungu vingine vinavyoashiria wajibu wa mzazi. Kifungu hiki ni lazima kitafsiriwe kulingana na wajibu unaotokana na haki za mtoto kwamba ana haki ya kuishi, kulindwa utu wake, heshima, mapumziko, uhuru, afya, elimu na malazi stahiki kutoka kwa wazazi wake.

Katika makala haya tunamwangazia namna anavyoathiriwa na ajira na kukosa haki zake za msingi mtoto anayeishi maeneo yanayozunguka migodi ya dhahabu wilaya ya Chunya mkoani Mbeya kusini Magharibi wa Tanzania.

Ajira kwa watoto ni jambo linalopigwa vita duniani kote, ili kuhakikisha kwamba jumuya ya kimataifa inafuata misingi na viwango vya kimataifa kuhusu ajira kwa watoto, ilitengenezwa mikataba kuweka bayana misimamo ya kimataifa.

Mkataba wa kimataifa wa mwaka 1989 unaujulikana dunia kote,uliopitishwa na baraza kuu la umoja wa mataifa ambapo Tanzania ilisaini mkataba huu julai 10 1999.

Mkataba wa Afrika wa mwaka 1999 kuhusu haki na wajibu wa mtoto inasisitiza kutokomezwa kwa ajira mbaya ya watoto. Lakini pamoja na mikataba hiyo, kuna mingine miwili ambayo lengo lake ni kuweka misingi inayolenga kuondoa ajira kwa watoto.

Nchi zinalizoridhia mikataba hiyo ikiwemo Tanzania zinawajibika kuhakikisha zinatekeleza wajibu huo na ni lazima ziweke misingi hii katika sheria za nchi zao, ili ziweze kuitekeleza kwa ufasaha zaidi.

Watoto wanaofanyishwa kazi katika machimbo hayo hususani wa watoto wa kike ndio wako katika hatari zaidi ya kubakwa, kupata mimba na kuolewa kwa nguvu kuingia katika ndoa za utotoni, ufikiaji wao wa elimu umekuwa duni.

Aidha kunyimwa haki yao ya kushiriki katika masuala ya kuwaendeleza, ushiriki wa watoto wa rika zote na hasa watoto wa kike umekuwa duni katika vijiji vya machimbo ya dhahabu katika wilaya ya Chunya hivyo wanakosa masuala mbalimbali yanayohusu kijamii.

Je, Serikali na wananchi imefanya nini kukomesha ajira za watoto migodini

Afisa maendeleo ya jamii Telesia Mwendapo licha ya kutokuwa tayari kuelezea bajeti ya iliyotengwa kwaajili ya kushughulikia ajira za watoto maeneo ynayozunguka migogidi,anasema suala la ajira za watoto ni changamoto kubwa.

Kutokana na watoto kutoka maeneo tofauti ya sangambi, makongolosi na kitoji cha mwaoga kuacha shule na kujiingiza katika shughuli hatarishi kama migodini na kwenye kilimo cha tumbaku ambako wanakwenda kuajiriwa katika mashamba ya tumbaku.

Anabainisha kuwa uwepo watoto wanao kukinzana na sheria katika wilaya ya Chunya kipindi cha mwaka 2016 wameweza kupata kesi 29 ambapo anasema kesi hizo ni wezi wa kuvunja kwa mabosi wanao waowaajiri,kubaka au kubakwa na watoto kuacha masomo.

Licha ya kuwepo kwa changamoto hizo lakini idara hiyo imeshindwa kujua kuna watoto wangapi wanafanya kazi migodini kutokana na bajeti iliyotengwa mwaka 2015/2016 ambazo hata hivyo hakutaka kutaja kiasi kushindwa kutekelezeka.

Katika kupunguza ajira za watotO migodini maeneo tofaitu wilayani hapa Mwedapolea anathibitisha kuwa wamekwishapata wafadhiri ambao ni mashirika yasiyo ya kiserikali UNICEF na PSI ambao wameridhia kushirikiana na halmshauri katika kutafuta takwimu na kuhakikisha watoto waliko migodini na maeneo ya mashamba ya tumbaku wanalejeshwa shule na wengine vyuo vya ufundi.

Diwani wa kata ya matundasi Kimo Choga anathibitisha kuwepo kwa watoto wanaojiajiri na kuajiriwa katika maeneo ya machimbo ndani ya kata hiyo na anakiri kwamba serikali haijawajibika kuchukua hatua yeyote kuzuia kasi kubwa ya ajira za watoto.

“Kata hiyo kuna watoto wengi wanaojihusisha na shughuli za machimbo, wengine wanafanya uchuuzi wa kuzungusha biashara ndogo ndogo kama kuuza karanga, mayai na matunda, na katika muda wote nilioishi hapa hata siku moja sijawahi kuona shirika lililofika kwaajili ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya ajira za watoto” anasema Choga.

Choga anasema kutatua ajira hizo za watoto migodini katika kata hiyo imekuwa vigumu kutokana na asilimia kubwa ya wananchi hapo kutegemea uchimbaji wa madini ya dhahabu na kudai kuwa kupunguza yeye kwa nafasi yake amekuwa akiwaelimisha wananchi kuwa si vizuri kumuajirimtoto kwenye shughuli hizo za uchimbaji wa dhahabu.

Mhandisi Nuru Shabani ni mkaguzi wa migodi na baruti katika ofisi ya madini wilaya ya Chunya, anasema Chunya kuna wachiimbji wadogo wadogo wa madini ya dhahabu zadi ya 4000 kati ya hao wenye leseni ni 1102, ambao kati ya hao kuna leseni zinzomilikiwa na watu binafsi ni 1005 na zinazomilikiwa na makampuni ni 197 na pia wanaleseni za uchimbaji wa kati mbili.

Akizungumzia suala la ajira za watoto wilayani Chunya anasema kuwa kuna changamoto kutokana na asilimia 80 hawana leseni kiasi ambacho kudhibiti ajira za watoto ina vigumu kwani wachimbaji wengi wanachimba kiholela na kukiuka sheria ya madini ya mwaka 2010 inavyowata kuwa kila mmiliki wa leseni anatakiwa kuwa na meneja na kuangalia usalama afya mahahala pa kazi vitu ambavyo wachimbaji hawafanyi

Anasema kuthibiti ajira za watoto ambapo wanajihusisha na uchimbaji inakuwa ngumu kutokana na wachimbaji walio wengi kutokuwa na leseni kwani walio na leseni aslimia 20 hivyo kunahitajika ushirikiano kutoka katika serikali za vijiji na na wanachi kwa ujumla.

Mkuu wa wilaya ya Chunya Rehema Madusa amekiri kuwepo kwa ajira za watoto kwenye wilaya yake na anasema si kwamba kwenye machimbo ya dhahabu tu ndio kuna tatizo hilo lakini kwenye kilimo cha tumbaku na maeneo ya glosari ambapo ameeleza kuwa kupitia idara ya maendeleo ya jamii walishaanza kulishughulikia suala la ajira za watoto na kwamba tangu januari hadi juni mwaka 2017, wameisha wabaini watoto 78 na watoto 48 tayari wamerudishwa shuleni na waliobakia idara ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na wafadhiri ambao ni Unicef kutokana na kutokuwa na sifa za wenda sekondari wameweza kuwapeeza katika vyuo vya ufundi.

“Anasema jamii lazima ishirikiane na serikali kukomesha suala la ajira kwa watoto kwani wao wanajua wapi watoto hao wanafanya kazi”,alisema Madusa.

Mratibu Elimu Kata Ayobu Mwangosi katika kupunguza ajira za watoto katika kata hiyo wameweka utaratibu kudhibiti utoro ambapo kwa mtoto ambaye hajafika shuleni anawajibika kulipa shilingi elfu hamsini(50,000).

Mashirika yasiyo ya kiserikali yamefanya nini?

ELIMISHA ni shirika lisilo la kiserikali, lililoanzishwa na baadhi ya waandishi wa habari mwaka 2009. Kwa lengo la kusadia juhudi za serikali za kuwezesha jamii katika Nyanja za utatifiti, utetezi, kujenga uwezo na kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari na mbinu nyingine.

Festo Sikagonamo ni mkurugenzi wa shirika hilo anasema ELIMISHA limejielekeza zaidi katika kusadia makundi ya Wanawake, Watoto na Vijana kuwa na Afya, Elimu bora, kushiriki na kushirikishwa katika shughuli za maendeleo ya nchi, ili kuwa na maisha bora, endelevu na yenye kutimiza ndoto zao.

Anasema katika ufuatiliaji wa shughuli zao za vijijini yakiwemo maeneo yakiwemo maeneo ya machimbo ya madini ya dhahabu, Elimisha ilibaini kwamba wakati uchumi unapoyumba katika eneo watoto wanaotoka katika jamii zenye kipato cha chini wanakumbana na tishio kubwa katika mstakabali wa maisha yao ndani ya kaya mbalimbali.

“Mara nyingi, jambo hili huanza kuwadhuru watoto hawa wakiwa wangali wadogo na hadi wanapofikia katika kiwango cha shule ya msingi, Katika mfumo wa elimu Tanzania na baadhi ya nchi za afrika, watoto hao hupata tishio kubwa zaidi, ya kutopata gredi nzuri shuleni na hata kukosa kumaliza masomo yao ya shule ikilinganishwa na watoto wengine wanaotoka katika familia zenye uwezo kiuchumi” anasema.

Anasema “ hata Elimisha ilianzishwa kutokana na msukumo wa wanahabari uliosababishwa na mguso walioupata katika utendaji wao wa kazi za kila siku. Katika kutekeleza majukumu yao yakutafuta na kusambaza habari, waanzilishi wa shirika hili, wanapata fursa ya kuyafikia maeneo mengi yakiwemo ya vijijini, ambapo wanajionea na wanashuhudia matatizo ya kijamii yakiweo ya watoto” .

Katika hali hiyo waliweza kuona uwepo wa changamoto, upungufu na pengo ambalo lisingeweza kuzibwa kwa kutafuta na kuandika habari peke yake, na hivyo kuona umuhimu wa kuanzisha shirika hili" anasema Sikagonamo.

Anasema kuna ukiukwaji wa haki za watoto, kuna kundi kubwa la watoto ambao ndiyo mustakabali wa taifa wakiwa wamekosa matumaini, baadhi yao wanakosa fursa za elimu kutokana na wazazi kutothamini elimu, wengine wanatumikishwa kinyume cha sheria katika migodi yenye leseni na isiyokuwa na leseni, kutumikishwa katika mashamba makubwa, kufanya vibarua vya kubeba mizigo, kuchunga mifugo, na kazi za ndani hali ambayo inawaathiri kisaikoloji katika maisha yao. Aidha yatima, ambao idadi yao inazidi kuongezeka kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, wameachwa bila msaada.

Anasema kuna mambo kadhaa yanayoeleza sababu za wanafunzi kuwa na mazoea ya kuacha shule kwa watoto walio toka katika familia zenye rasilimali kidogo, tishio linatokana na sababu kama vile viwango vya watoto waliovunja sheria, viwango vya juu vya watoto waliopata mimba, wakiwa wadogo na kutegemea kiuchumi mzazi au wazazi wenye mapato ya chini.

Ambapo anasema hii inatokana na familia au jamii zisizotilia maanani uwekezaji katika elimu na maendeleo ya watoto maskini hupata matokeo yasiyo mazuri kwani baadaye watoto hawa hukosa kazi na huwa na vipato vidogo, Viwango vikubwa zaidi vya kuzaa mapema na hatari zake kwa familia, afya na maisha bora kwa ujumla ndiyo mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa kwa kuwa elimu kutoka kiwango cha shule ya msingi hadi shule ya sekondari ina umuhimu mkuu maishani.

Watoto wanatoka katika kaya maskini hawapati huduma muhimu, hii inawafanya wakose kwenda shule kwa siku nyingi katika kila mwaka Pia, tafiti mbalimbali zinaeleza kwamba kuna uwezekano zaidi kwa watoto maskini kuteseka kwa njaa, uchovu, kukasirika ovyo, maumivu ya kichwa, maambukizi ya masikio, mafua na homa. Magonjwa haya yana uwezo wa kumzuia mtoto au mwanafunzi kuelewa yale anayofunzwa darasani.

Pia anasema maeneo yaliyoathiriwa sana na umaskini mara nyingi yanaweza kuwa na ukatili mwingi, "Katika maongezi na baadhi ya watoto, walisema kuwa, baadhi ya watoto wengine hawasomi vizuri darasani hasa wale wa kutoka jamii maskini katika maeneo yenye makazi duni walisema kuwa wanashuhudia baadhi ya wenzao wakiwa wamekosa ari ya kusoma kutokana na kutokuwa na uhakika wa chakula nyumbani kwao.

Watoto wenye umri mdogo wa chini ya miaka 10 wanafanya kazi katika baadhi ya migodi midogo ya dhahabu wilayani Chunya, wanakabiliwa na hatari kubwa kwa afya na hata maisha yao. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine inapaswa kukomesha ajira kwa watoto.

Je,ni hatua gani zilizozichukuliwa na shirika kukomesha ajira za watoto?

Mkurugenzi wa Elimisha anabainisha kuwa wamekuwa wakitayarisha vipindi vya Redio vinavyohusu utetezi dhidi ya watoto kuishawishi jamii pamoja na wadau wengine kuchukua hatua, wakiwa

wananajua kwamba Serikali ya Tanzania inazo sheria nzuri zinazozuia ajira kwa watoto, ingawa kuna changamoto kwenye suala la usimamizi wa kutekeleza sheria hizo.

“ Tunathubutu kuishauri serikali na wadau wengine kwamba migodi inayoshirikisha watoto wadogo katika shughuli za uchimbaji madini ni vema inayang’anywe leseni, wachimbaji wafuate sheria na taratibu, watoto kushiriki katika shughuli za uchimbaji ni makosa”.

Hata hivyo kama jamii inayozunguka maeneo ya migodi haibadilika na kuchukua tahadhari juu ya ajira za watoto migodini tunaweza kuzalisha jamii ambayo haiwezi kuwa na taifa lililo bora.

MWISHO.